j) i) Chuma – chumo, Uchumi , mchumi, mchuma (al. 2)
ii) Pake – mpaka , mpakaji, upakaji , upako.

k) Jisimba liliingia katika jumba na likafumwa. (al. 2)
jikuku

l) /gh/ /na/

m) Kipozi – Runinga
Kitondo – mwalimu
Ala / kitumizi – kwa toroli (al 3)

n) kiunganishi kilete maana ya kwa kuwa / kwa sababu

o) i) Nyama – i - i (al. 1)
wema - u- u (al. 1)

p) ✓“ah!✓Huu✓ndio mkutano uliotuitia? ” ✓ Mmoja✓ wao akaropoka. Alama ½ x 6 = 3

4. **ISIMU JAMII**

a) I – Kiswahili ni lugha ya mseto – zao la kuingiliana kwa lugha za kigeni na lugha za Afrika Mashariki.

II - Tokeo la ndoa baina ya wanawake wa pwani wa Afrika mashariki na waarabu

III - Kiswahili ni lugha ya kibantu. **(alama - Kila hoja al 1x 3 = 3)**

b)
- Kusisitiza ufundishaji wa Kiswahili katika ngazi zote
- Kuunda taasisi ya kitaifa ya uchumi wa Kiswahili.
- Serikali ifadhili maendeleo ya lugha ya Kiswahili
- Kuanzisha mashindano ya uandishi wa Kiswahili nchini
- Uchapishaji wa vitabu zaidi vya Kiswahili.
- Vyombo vya habari vitumie Kiswahili sanifu kwa wingi
- Uchapishaji wa magazeti na majarida zaidi ya Kiswahili.
- Serikali ibadilishe sera zake kuhusu lugha ya Kiswahili.
- Kiswahili kitumike kwenye mtandao

(Hoja zozote saba 7 x 1 = 7)

102/2

KISWAHILI KARATASI YA 2 LUGHA

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
MUJARIBU WA MWIGO WILAYA ZA BOMET/CHEPALUNGU
JULAI / AGOSTI 2010

SEHEMU A: UFAHAMU

1. a) Hawakuweza kujikinga na haieleweki walivyookoka uvamizi
   b) Wanyama hatari waliishi humo
   c) (i) Uwezo wa kutumia silaha kujikinga na kupata chakula
      (ii) Uvumbuzi wa moto ulimwezesha kuishi pangoni
   d) (i) Walitembea kwa kuinama
      (ii) Walikuwa na nywele nyingi mwilini
   e) (i) Walipohisi, walipoona, walipokumbwa
      (ii) Kujitetea, kujilinda
      (iii) Makaazi, makao, nyumbani

SEHEMU B: UFUPISHO

a) Manufaa

Hutumika kama nyenzo ya kufundishia

Hufanya watu kuchua “misuli” ya kibongo na kufanya watu kuwa makini katika shughuli

Hutumbuiza na kuchangamsha. Hii hupunguza gharama na wakati wa kuandama chemichemi nyingine za burudani.

Huendeleza utamaduni, kaida na amali za jamii. Mengi yanayotokea katika runinga huwezi kuakisi mtazamo, mikakati amali za jamii. (alama2 kwa kila hoja na alama 2 kwa muwala)

b) Hasara

- Wakati mwingi huendeleza hulka ambazo huchukuliwa kama zinazofaa na zinazofuatwa na wastaarabu. Hivyo, vijana huziiga na kuzifuata.
- Runinga huweza kuwa kikwazo cha mawasiliano miongoni mwa familia. Haya yanaweza kuwafanya baadhi ya wanafamilia kujitenga. Waliojitenga huwa rahisi kuingisha maovu.
-Baadhi ya matangazo ya runinga hupotosha na kuwafanya watu kushiriki katika mambo hatari kama vile ulevi na kuvuta sigara.
- Huwafanya watu kuiga tabia ya matumizi za nguvu za mabavu. (alama 2 kwa kila hoja na 2 kwa muwala)

SEHEMU YA C

1 Sauti za ufizi:- t, d, n, s, z, l, r. Zozote nne

2. a) Shadda- Hutumiwa kueleza ile nguvu inayosikika wakati wa kutamka silabi
   b) Kiimbo- Ni mpando au mshuko wa sauti wakati wa utamkaji wa sentensi

3. Umuhimu wa kiimbo
   - Hutumiwa kuashiria muundo wa kisarufi yaani kuonyesha sentensi, vishazi na mipaka mingine
   -Hisia za kibinafsi za msemaji kama kuridhika, dhihaka au dharau, hasira na kadharika.

4. a) Kitenzi jina au nomino za vitenzi vya ngeli ya KU-KU
   b) Hutumiwa kama kiwakilishi cha nafsi ya pili (wewe)

5. a)- Kutenganisha jina la muhusika na maneno anayosema katika mchezo wa kuigiza kwa mfano. Mbura: unataka nini?
- Kutangulia kwa orodha Fulani k.m ligi ya uropa inachezwa na timu maarufu sana: Manchester, Chelsea na Liverpool
- Kutangulia maelezo k.m mama alipomaliza kusema kwa simu alianza kurukaruka kwa furaha: haikosi alikuwa ameadhidiwa tunu. (Zozote mbili)


b) Kutenganisha silabi za maneno kwa mfano ni-na-shu-ku-ru.
-Kuonyesha kuwa neno halingetoshea nafasi katika mstari na hivyo linaendelea katika mstari unaofuata k.m vile- Kujulisha
-katika maneno, hasa vivumishi ambavyo huchukua viambishi vya ngeli k.m-o-te,-o-o-te n.k
-Kutenganisha maneno ambatanishi k.m Isimu- jamii
-Katika tarakimu ili kutenganisha mwanzo na mwisho wake k.m 2002-2006
-Kudumisha sauti hasa wakati neno linapotamkwa (Zozote mbili)

6. Ni kile ambacho hukiweza kuchukua kiambishi cha nafsi au ngeli na kile cha wakati au hali. K.m baba yungali kitandani. (ngali)

7. Hufafanua vitensi kwa kurudiarudia neno moja mara mbili. K.m Yohana amelala kifudifudi n.k

8. Kiongozi mmoja alisimamia kura kwa niaba ya mwenzake, naye baadaye alisimamiwa na yule aliyesimamia alipopumzika.

9.





N v

Yule mwalimu amevunaa mahindi mengi

10. - Mwanawe- shirikisho kitondo
    - Baiskeli- shirikisho kipozi
11. " Ni muhimu mujitolee kazini kwa sababu taifa la kesho linawatengemea ninyi," Kiongozi aliwakumbusha raia.
12. a) Watoto walitekwa nyara
    b) Mwizi amekufa amelala tu
13. Kuta zilizojengwa zimepomoka
14.- Toto limefunga lango la jumba lao
    - Matoto yamefunga malango ya majumbo yao
15. Jenga – jengamana
    - Ganda – gandama
16. a) Chagizo- Alfajiri na mapema
    (b) Kazi
17. Ada ya mja hunena muungwana ni kitendo.

SEHEMU YA D: ISIMU JAMII

Mwalimu kuhakiki majibu.

TATHMINI YA PAMOJA WILAYA ZA BORABU-MASABA – 2010
102/2
KISWAHILI

KARATASI YA 2
LUGHA
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. a) Ilikuwa nyuma.
Sababu. Haikuwa na bandari wala viwanja.
(alama 2)

b) Ni vema, la sivyo malezi yake yatakuwa magumu.
(alama 2)

c)
i) Ikiwa ulimwengu haungeumbwa mapema, wakaaji wake hawangepata mahali pa kukaa.
ii) Kwa biashara ya vitabu kustawi watu ni lazima wafunzwe kusoma mbele la sivyo vitabu vizuri vitaonekana vibaya.
iii) Watu wasipofunzwa utukufu wa dini kabla ya kujenga msikiti, utaonekana kama mkahawa mchafu.
(3x1= 3)

d) Wananchi hawatafikiwa na vyombo/hawatapata maendeleo.
(2)

e) Ilikuwa na washauri wabaya wenye mapuuza.
- Haikuwa na vyombo, viwanja au njia/barabara.
(2x1=2)

f) Kila azimio katika maisha hutaka neno fulani kufanywa kwanza ili kuyashawishi maendeleo yake
(2)

g)
i) Kutumaini/kutaraji/kutegemea
1
ii) hamu ya kujua/kufanya jambo
1

2. a)
i) Kila jambo tufanyalo kuhusiana na lugha hustawisha ufahamu wetu.
ii) Mazoezi ya kuandika hustawisha ufahamu wa kusoma.
iii) Twajifunza matumizi ya lugha katika kuzungumza na kuwasikiliza wengine.
iv) Lugha iliyoandikwa ni aina ya mazungumzo.
v) Ujuzi mwingi katika kuzungumza hupatikana shuleni.
vi) Ujuzi wa kila siku husaidia katika maendeleo ya kusoma na msamiati.
vii) Husaidia kufahamu yaliyoandikwa.
viii) Hali ya mwanafunzi (pia) ni ujuzi.
(8x1=8)

b)
i) Karibu elimu yote imeandikwa vitabuni.

ii) Lugha zote hazina ustawi sawa.
iii) Zingine hazina vitabu vingi/zina vitabu vingi.
iv) Mwanafunzi anayesoma afaa kusoma mengi kando na taaluma anayoisomea.
(4x1=4)

$$M^{a8}_{b4}$$
$$u_{t}-{}^{3}\!/_{15}$$

3. a) - Kutolea rai/wazo
- Kuuliza swali
- Kuonyesha amri
- Kuonyesha mshangao zozote
(3x1=3)

b) M – tu – mbwi – ni (4x ½ =2)

K KI KKKI KI

c) i) Serikali ilitutoza kodi kubwa.
ii) – Mbili ni jawabu/jibu la tano ondoa tatu.
- Mbili ni masailio ya……
(2x1=2)

d) i) chafua/chafuka/chafuliwa/n.k.
ii) kopa/kopwa/kopana/n.k. (4x ½ =2)

e) S ⟶ FN+FT
FN ⟶ N_1+U+N_2
N_1 ⟶ Mama
U - na
N_2 - Baba
F_I – T+E
T - wako
E – Mtini (8x ½ =4)

f) – Sisi na yeye – mofimu za nafsi huru
- tu-na-m-penda (tu na m-nafsi tegemezi) (4x ½ =2)

g)
i. Kiunganishi
ii. Wakati uliopo
iii. Kauli ya kutendana k.m. pigana
iv. Kuonyesha umilkaji k.m ana pesa
v. Kuonyesha nafsi ya kwanza umoja k.m. naondoka (ninaondoka), nami (na mimi), n.k
vi. Kuonyesha mtendaji k.m alipigwa na polisi.
vii. Kuonyesha mfulilizo wa matukio k.m waliwasili na kutupiga na kuondoka.

viii. Kuonyesha hali k.m ana hasira. (zozote 3x1=3)

h) Sentensi iwe moja na ionyeshe:
i) Ngoma – ala ya muziki / Musiki wenyewe
ii) Goma – Susia kutenda jambo

i) A – Kiambishi kiwakilishi cha nafsi
ku – Kiambishi kiwakilishi cha mtendewa.
C – Kiambishi cha kauli/mnyambuliko .
A – kiishio/kimalizio. (4x ½ =2)

j) Fundi mzuri – KN/FN
Ni aliyetualika kwake – KT/FT
(2x1=2)

k) i) Umilikaji
ii) kusistiza
(2x1=2)

l) atumie: wa au za k.m. uta wa baba…..
(alama 2)

✓ ✓ ✓ ✓

m) Jibwa letu limekatwa jikia/kia/
Jijibwa letu limekatwa jijikia (4x ½ = 2)

n) Hali isiyodhihirika (ya wakati uliopo)
2

o) Unywele wake ulinyolewa wote (4x ½ = 2)

p) i) Hali wala kulaani
ii) Asiponiona sitamfurahisha.
(2x1=2)

q) <u>Ukila</u> sana utakuwa <u>mgonjwa</u>
(2x1=2)

r) i) lana
ii) liliana
(2x1=2)

4.
i. Dini

ii. Biashara
iii. Mafunzo na utahini shuleni
iv. Vyombo vya habari
v. Ndoa baina ya watu wa jamii tofauti
vi. Siasa
vii. Bunge
viii. Uandishi – vitabu
ix. Kufanywa lugha ya taifa/rasmi
x. Mijadala na hotuba
xi. Chombo cha utawala.
xii. n.k. (zozote 5 zilizoelezwa 5x2=10)

Kutaja = 1
Maelezo = 1

102/2
KISWAHILI KARATASI YA PILI LUGHA
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
MUUNGANO WA SHULE MBALIMBALI MTIHANI WA KUJITATHIMINI JULAI / AGOSTI 2010

SEHEMU YA A: UFAHAMU (ALAMA 15)

1. Ajali hutokea bila kutarajia (AL 2)
2. Hutokana na ajali wasizofikiria watu wengi kama vile kuteleza msalani
   Aidha wengine huteleza walipokanyaga vitu vyenye unyevu sakafuni.
   Watu wazima na watoto hulemazwa na ajali hizi. (alama. 3)
3. i) Watu wanapozama katika shughuli au kupata jazba ya kutenda kazi
   ii) Kuubeba mzigo wenye uzani usiokadiriwa.
   iii) Ukiwa umepanda juu ya kibao kuangika picha ukutani.
   iv) Ajali kutokana na vifaa vya nyumbani k.v visu, meko ya gasi, mashine zinazotumia umeme n.k (al 3)
4. i) Kukuza tabia na mazoea ya kuwa waangalifu nyumbani.
   ii) Ni vizuri kupata ujuzi wa jinsi ya kutumia vifaa na kuhakikisha tunavirusha ipasavyo
   iii) Kuwepo kwa vifaa pamoja na uwezo wa kutoa huduma ya kwanza
5. i) Jazba - Msisimko / msukumo / hamu kuu
   ii) Makasri - Majumba ya kifahari
   iii) Makovu - Alama/mabaka yatokanayo na majeraha.
   iv)Kuepua - Kutoa kitu mekoni

***2.* SEHEMU YA B: UFUPISHA (ALAMA 15)**

a) (i) Dawa za kulevya zinaweza kugawika katika makundi mawili makuu: dawa hasi na dawa sugu.
(ii) Dawa hasi huwa na matokeo hasi kwenye mwili wa mtumiaji
(iii)Dawa sugu humchangamsha mtumiaji na kumfanya apandwe na nishati za ajabu.
(iv)Huzitekenya seli za ubongo wa anayehusika. (al 6) (utiririko al 1)
b)-Kwanza, dawa za kulevya huzichangamsha seli za ubongo kwa kiasi kikubwa

-Mwili wa mhusika hukosa hisia kutoka viungo vya mwili au misuli ya mwili.
-Hutenda mambo kupita kawaida yake. Hali hii hiutwa ' mpumbazo”
-Pili, huwa mchovu, hulala kupita kiasi, hukosa hamu ya kazi na kupuuza maswala ya siha
- Aidha huwa msahaulifu, hupungukiwa na kumbukumbu na kuwa na hisia za uhasama na jamaa na hivyo kujitenga.
-Hatua ya tatu huwa isiyo ya kawaida
Mtumiaji hujitenga kabisa na jamaa yake.
- Seli za ubongo huwa zimeharibikiwa na hivyo kuonyesha uchukuvu kwa vitu kwa kupigana na kuchanganyikiwa.
-Hushikwa na magonjwa ya kiakili/ mwendawazimu.
-mwisho, hufariki.***Zozote 7 x 1 Al. 7 (Utiririko (al.1)***

3. MATUMIZI YA LUGHA

a) Kadiria sentensi ya mwanafunzi almuradi imetangulizwa kitenzi - jina. K.v kucheza, kuimba n.k (al 1)
b) Kuchoka kitenzi-jina (alama 1½)
Ndiko - kusisitiza/kurejelesha/ kitenzi kishiriki kipungufu(l/2
Kulimfanya kitenzi(l/2
Kujihami - kurejelea(l/2
c) i) Kivumishi - Nguo nadhifu zimeanuliwa. (alama 1
ii) Kielezi - amevaa kinadhifu(al 1)
d) Mwanasiasa aliyeshindwa hakutoka nje kwa hasira wala kuacha uchaguzi ukiendelea. (al 2
e) S— SI+U+S2 S2.... KN +KT
SI ....NN I KT KN.....
KN……N N.....Mtoto
Nl.....Nyanya KT.....T+N
KT.....T+N2 T .....Anakunywa
T .....Anakunywa N.....Uji
N2 .....Maziwa
U....Lakini (Alama 4)
f) Alikuwa ..... Ts(alama 1)
Akivaa..... T(Alama 1)
g) i) Wakati wowote (alama 1)
ii) Wakati maalum (Alama 1)
h) Kadiria k.m Mwanafunzi aliyekula chakula/ ameshiba. Tegemezi.....Huru
(al 1 (al 1)
i) i) Kuja - njooni!(al 1)
ii) Leta - Leteni (al 1)
j) i) Mtoto alimwita mamake aende akaone ndege (alama1)
ii) "Gombeeni nafasi za kisiasa!" Kiongozi aliwashurutisha akina mama. Au “Akina mama mgombee nafasi za kisiasa!" Kiongozi akawashurutisha. (alama 1
k) Kadiria. K.m
Mama (Nl) + yule(Vl)+ mfupi(V2) + ameenda(Tl) + sokomo(N3) + kununua(T2) + mboga (N3)
1) i) Hali ya vitu viwili au zaidi kugusana na kukaa hivyo kwa muda mrefu. (al 1)
ii) Kuonyesha mshikamano(al 1
m) i) Kiongozi wa kiume katika kikundi cha wanawake.
ii) Neno linalotumiwa na wanawake kuitana

iii) Kipimo cha kitambaa
iv) Sura ya kitabu/buku
v) Ugonjwa wa watoto

n) Mtoto mkembe (mdogo) amebeba mkebe wa mafuta.(kadiria)(ala 2)

o) Kijijana kile kilipewa kijipande cha kijikate na kisichan kirembo.(al 1)

p) i) Kimadende**……**r(al 1)
ii) Kitambaza ——— l(al 1)

q) Kadiria k.m
Mama alimpikia mgeni chakula janajioni.
kitondo kipozi chagizo
(al 1) (al l) (al. 1)

r) Mtoto msichana alilia kwa huzuni (alama 1)

s) Safari yangu haikuwa na ugumu wowote kwa vile nilikuwa nimejitayarisha. (alama 2)

t) i) Izara - Fedheha/ Aibu/Dosari(alama 1)
ii) Anisi Furahisha/ pumbaza/ fariji (al 1

u) i) Maziwa yote yamenywewa na watoto(alama 1)
ii) Yule mzee aliyemwoza msichana wake kwa mzee ameshtakiwa. (alama 1)

4. ISIMU JAMII ALAMA 10

a) i) Kiswahili kilichipuka kwa sababu ya ndoa kati ya wageni na wenyeji.
Uongo kwani kila ndoa ya watu tofauti inapotokea hapachimbuki lugha mpya.
(hoja 1x1 maelezo 1x1

ii) Lugha ya watoto waliotokana na ndoa hizi za mseto.
Uongo maana watoto wa ndoa za mseto hujifunza lugha ya mama au baba. Hawawezi kuzikaidi lugha hizi mbili na kuza yao. **(hoja 1x1 maelezo 1x1**

iii) Lugha ya kibantuUkweli uchunguzi wa malcolm Guthrie inaonyesha kuwa ina mizizi 22000 kutoka kwa lugha 200 za kibantu ambayo inafanana. Kiswahili ni miongoni mwa lugha hizi.

(hoja 1x1 maelezo 1x1

b) i) Hutumiwa na watu wengi katika shughuli za kila siku.
ii) Huwa imeenea sana.
iii) Ni lugha ya mama/kwanza ya kikundi fulani cha watu katika taifa husika
iv) Ina muundo wa kiisimu unaofanana na ule wa baadhi ya lugha za watu katika taifa husika.
v) Kujifunza ni rahisi k.v. kiswahili na lugha zingine za kibantu.
vi) Ilete hisia za kizalendo na utaifa. vii) Isiwe ya kigeni. **(hoja zozote 4x1**

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
102/2 2010

1. UFAHAMU

a) i) Ufisadi
ii) Uongozi mbaya
iii)Turathi za kikoloni
iv) Uchumi kuegemezwa kwenye kilimo kinachotegemea mvua isiyotabirika
v) Idadi kubwa ya watu inayoupika uwezo wa uchumi taifa linalohusika
vi) Ukosefu wa nyenzo na mali za kuwakwamua raia kutoka lindi la umasikini
vii) Ukosefu wa elimu na nafasi za ajira (4x1=4)

b) Asilimia kubwa ya pato la kitaifa katika mataifa mengi hutumika kuyalipa madeni hayo. (1x2=2)

c) i) Kuibuka na mikakati bora ya kupambana na umasikini
ii) Pawepo na sera zinazotambua ukweli kuwa asilimia kubwa ya raia wa mataifa hayo ni masikini
iii) Kuzalisha nafasi za kazi kwa dharura
iv) Kupanua viwanda hususan vinavyohusiana na zaraa ambayo ni tegemeo kuu la mataifa mengi
v) Kuendeleza elimu
vi) Kuimarisha miundo msingi (4x1=4)

d) Ni chanzo cha kufa kwa viwanda asilia na kuendeleza umasikini zaidi (1x2=2)

e) i)kulitadarukia – kulishughulikia, kulitatua kulikabili
ii) Kuatika - kuanzisha , kutia , kuzua
iii) Kuyaburia madeni. Kuyasamehe madeni, kuyaondolea madeni (3x1=3)

2. UFUPISHO

a) i)-Rafiki mweye sifa nzuri
ii)-Kupendanahata kama hakuna pesa au zawadi
ii)-Urafiki wa kubadilishana mawazo mbalimbali
iv)-Kuzingatia ukweli na uaminifu
v)-Rafiki mwenye umri sawa
vi)-Rafiki mwenye umri mkubwa hamuwezi kushirikiana naye ipasavyo
(kila hoja alama 1 jumla alama 6)

b) i) Kutozingatia mambo kama utajiri tunapochagua marafiki
ii) Urafiki huenda ukaharibika wakati wowote
iii) Waweza kuwa matatani ikiwa pesa za tajiri ni haramu
iv) Lakini waweza kuwa na rafiki tajiri bila kuzingatia mali yao
v) Urafiki ni hali inayojengwa kwa muda na utaratibu
vi) Kukosana baina ya marafiki ndiko kujuana
(kila hoja alama 1) (utiririko alama 3)
(jumla alama 6)

3. MATUMIZI YA LUGHA

a) (i)/w/,/y/ (2x1=2)
(ii) /k/ /sh/ (2x½=1)

b) Yambwa tendwa – josho
Yambwa tendewa – wanakijiji (2x1=2)

c) Nilimjibu (kuwa / kwamba) singeenda sokoni siku hiyo ila ningeenda siku iliyofuata
(6x½=3)

d) Wale – kiwakilishi kionyeshi / kiashiria
Wale – kivumishi kionyeshi / kiashiria
Wale - kitenzi

e) Hapo napo ndipo ninapotaka
Hapo napo ndipo nitakapo (yoyote 1x1=1)

f) S – KN +KT✓
KN – N + S✓

N – Mwanafunzi✓
S – anapohepa shuleni✓
KT – T + E✓
T – huadhibiwa✓
E - kikondoo✓ (6x½=3)

g) Kitoto cha kizee kile kiligongwa kwa kijundo kilipofukuzwa na kijibwa. (8x¼=2)
h) Alakulihali – kwa vyovyote vile.

i) "Matafanya kazi hii mpaka lini?" "Mzee alisema, "Nataka ikamilike leo, kesho mtaanza nyingine." (kutuza)

1- 0 2-½ 3-1 4-1 ½
5-2 6- 2½ 7- 3 8- 3½ 9- 4

j) Teo za Abunuasi zimepotea
Liwali wa kwanza amewasili shambani (2x1=2)

k) Rudini -wingi wa wahusika
ni -kitenzi kishirikishi kipungufu.
nitamtembeza – kiambishi kiwakilishi cha nafasi (kiambato/tegemezi)
mjini - kielezi

l) (i) Ebo! Kuonyesha dharau
(ii) kefule! Kinyume na matarajio (hasa kuhusu maadili) (2x1=2)

m) (i) wakati maalumu
(ii) Wakati wowote (2x1=2)

n) (i) Imewia wananch vigumu kuelewa katiba (1x1=1)
(ii)cha – chiwa (1x1=1)

o) (i)-o-ote
(ii)-ote (2x1=2)

p) Mimi pamoja na Baniani tulichezewa.
Yeye pamoja na Baniani walichezewa (2x1=2)

q) (i) Pamba (i) sufi ya mmea iliyo nyeupe na laini
(ii) chakula au masurufu ya wakati wa safari
(iii) visha mavazi mazuri ya kupendeza
(iv) tia urembo
(v) tayarisha au panga vitu kwa uzuri
(vi) kuwa mahali aghalabu watu au wadudu
(ii)bamba (i) kamata mtu kwa nguvu"baka"
(ii)ziba au zuia
(iii)bati
(iv) kitu chembamba chenye ubapa (bamba la upanga)

r) Wanafunzi wote watakaofanya mtihani watatahiniwa na mwalimu huyu. (1x1=1)
s) Ufisadi fisidi (1x1=1)

4. ISIMU JAMII
i. Lugha huwa na sifa za kisheria
ii. Aghalabu huwa na sentensi ndefu
iii. Lugha huwa sanifu na ya adabu
iv. Matumizi ya msamiati maalumu
v. Kuchang'anya na kubadilisha msimbo
vi. Sifa zinazodhilika k.v unyenyekevu na heshima m.f Bwana spika,mheshimiwa
vii. Urudiaji / uradidi wa baadhi ya maneno
viii. Kukatizana usemi
ix. Huwa na mtindo maalumu
x. Matumizi ya ishara

xi. Inaweza kutafsiriwa -kutaja 5x1=5, -mifano 5x1=5 jumla 10

TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA NYAMIRA KASKAZINI - 2010
102/2
KISWAHILI (LUGHA)

MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA

1. **UFAHAMU**

(a) Mabadiliko ya maisha/athari za kigeni/mitindo mipya ya kimaisha;, mavazi, chakula, afya nk.
Mazingira yanayobadilika – Sheria zinabadilika
Teknolojia, tarakilishi nk. Zozote 3 x 1 = 3

(b) Wanyama walifugwa kwa wingi
Misitu ilikuwa kocho
Watu walikuwa huru hata kuwinda na kukata miti Zozote 2 x 1 = 2

(c) Chakula kilipatikana kwa urahisi mno na bila malipo au gharama kubwa. 1 x 2 = 2

(d) Idadi kubwa/kuongezeka kwa watu duniani
Mazingira yanayobadilika mara kwa mara
Mchanganyiko au matumizi ya madawa mengi pamoja
Uchafuzi wa hali ya anga Zozote 3 x 1 = 3

(e) Vijana si sawa na wazee; watu wazima wana hekima, busara na tajriba ya maisha
Watu wa siku hizi hawawashindi wa zamani kimaisha 2 x 1 = 2

(f) (i) Maganda ya miti
(ii) Ovyo ovyo bila woga au vikwazo
(iii) Hazikawii; hazichukui muda ; hazihimili 3 x 1 = 3

2. **UFUPISHO**

(a) UKIMWI – Ugonjwa wa zinaa usiokuwa na tiba
Mama anaweza kumwambukiza mtoto, wakati wa kuzaa au kunyonyesha
Damu ikichanganyika baina ya watu ni hatari
Watu waepukane na UKIMWI kwa vile ni hatari
Vijana waonywa dhidi ya wazee waasherati
Mila zingine zimepitwa na wakati
Serikali ina sera mbovu kuhusu mila

Umaskini huchangia UKIMWI

Ni wajibu wa serikali kupambana na janga hili Zozote 6 x 1 = 6

(b) Watu kuelimika/kuelimishwa waepukane na maafa

Vijana waonywa kuepuka maovu

Vijana waenzi mila za jamii zao; wasitupe tamaduni/desturi

Watu watii wanayoambiwa na wakuu

Kuzingatia maadili

Kujiepusha na tamaa nyingi za ulimwengu

Kuwa na utu – kutahadhari na UKIMWI Zozote 6 x 1 = 6



a- 6

b- 6

ut - 3

15 – 3h – 3s – z

3. **LUGHA**

(a) Nilipowasili tu nilishika tama.

Nikashangaa, “Loo! Moto huo ulianza vipi na ulikuwa umesababishwa na nini?” Nilishikwa na bumbuwazi. Magoti yangu yakaanza kuchezacheza 12 x ¼ = 3

(b) (i) Jitu hilo lilinishtua sana usiku huo.

(ii) Majitu hayo yalitushtua sana usiku huo

- sentensi zaweza kuwa tofauti 2 x 1 =2

(c) S ⟶ SI + U + S2 4 x ½ = 2

S						
S^1			**U**	**S^2**		
KN	**KT**			**KN**	**KT**	
N	**V**	**T**		**N**	**T**	**N**

Baba	**anafyeka**	**nyasi**	**ilhali**	**mtoto**	**anaambua**	**viazi**

(d) Zainabu alishangaa kumwona Kagame ameketi peke yake amesononeka huku watu wengine wakistarehe. Kagame alimfahamisha kwamba hakuwa na mkasa wowote ila alikuwa anasumbuliwa na ugeni tu; hakuwa amepata rafiki au sahibu Alama 4

(e) (i) Mtume aliyefika ni mrefu
Mitume waliofika ni warefu
(ii) Twiga hutimka/ hukimbia mbio ingawa ni mrefu 2 x 1 = 2

(f) (i) Nyuta zizi hizi ndizo walizotumia kuwafuma swara
(ii) Ugomvi wao ulisababisha kutalikiwa kwao 2 x 1 = 2

(g) (i) Kufuata, mfuasi, mfuatano
(ii) Kuzika, maziko, mzikaji, mazishi 4 x ½ = 2

(h) (i) Kuhofia isitokee kuwa hivyo
(ii) Kutokuwa na uhakika; kukisia 2 x1 = 2

(i) (i) Kitabu chochote kikipendwa na wasomaji wengi huwa maarufu
(ii) Askari yeyote apitaye hapo humchapa 2 x 1 = 2

(j) Alifika nyumbani, akaketi kisha akapiga simu Zozote 2 x 1 = 2

(k) (i) Kijiuta
(ii) Kijijiko 2 x 1 = 2

(l) (i) Kata – Eneo la kusimamia watu
- Kifaa, hasa cha kuchotea maji
- Hali ya kutenganisha k. m. uhusiano
(ii) Ua – fisha au toa uhai (kitenzi)
- Pambo (wingi maua) (nomino: LI – YA)
- Eneo lizungukalo nyumba au boma (wingi nyua – U – ZI) 4 x ½ = 2

(m) Ua wako wanuka kwa sababu huutumii kwa uangalifu 4 x ½ = 2

(n) Changu, letu, mwangu 1 x 2 = 2

(o) Wakati ujao, hali timilifu 2 x 1 = 2

(p) Sidhani kuwa kichapo pekee kingepelekea Manoti kulazwa hospitalini ingawa hakika Mogeni alimcharaza mno Alama 2

(q) (i) Kuvamia au kutia mikononi au kuficha kwa nia fulani

(ii) Kuota au kufikiria yasiyowezekana haraka 2 x 1 = 2

(r) Mtego wa panya huingia waliomo na wasiokuwamo 1 x 1 = 1

(s) (i) Waimbaji wasio maarufu hawajapata tuzo

(ii) Mama alitema dawa yote

4. **ISIMU JAMII**

(a) Sifa za lugha rasmi:

- Hutumika katika masuala rasmi; ofisini, bungeni, Kortini n.k.
- Yaweza kuwa lugha ya taifa
- Yaweza kuwa au isiwe sanifu
- Hubeba msamiati mwafaka au tosha k.v. katika nyanja za sayansi na teknolojia
- Haifungwi, haipendelei ukabila
- Huwa na utaratibu maalumu/spesheli 6 x 1 = 6

(b) Sajili ya vijana

- Huchang'anya msamiati
- Huenda na umri
- Hutofautiana kimaeneo
- Si sanifu moja kwa moja 4 x 1 = 4

102/2
KISWAHILI
Karatasi ya 2
LUGHA

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
WILAYA ZA KISUMU KASKAZINI NA MASHARIKI
JULAI / AGOSTI 2010

1.Ufahamu. (**alama 15)**

a) (i) Tofauti za rangi
(ii)Tofauti za kitamaduni
(iii) Hali ya kiuchumi
(iv)Uana / jinsia (hoja zote 4x1=4)

b) Hali ya watu wanavyoishi;tabia,mila na desturi zao,ustaarabu wao.
(hoja 1x2=2)

c) Ubaguzi wa sasa upo kati ya matajiri na maskini. Wenye hali nzuri kiuchumi hujiona bora kuliko wale wa hali ya chini. (alama 2)

d) (i) Utamaduni wa kiafrika umechangia katika kumdhalalisha mwanamke. Nafasi yake ni pale jikoni.
(ii)Taasubi za kiume.
(iii)Dini-ambayo inamweleza mwanamke kuwa yuko chini ya mme.
(iv) Mwanamke hajajikomboa kimawazo.Anajiona hana uwezo/ni kiumbe dhaifu
(hoja zozote 3x1=3)

e)Nchi nyingi haziwezi kupiga hatua kimaendeleo. Husababisha migogoro/migongano miongoni mwa wanajamii/kutoelewana kati ya wanajamii. (alama 2)

f) (i) Ubaguzi:Utengano unaotokana na sababu mbalimbali.
(ii)Masalia:Mabaki. (alama2)

Makosa:

Sarufi – usiondoe zaidi ya nusu ya alama alizopata katika kila kijisehemu.

Tahajia – Ondoa makosa 6 yaani alama 3 katika sehemu nzima ya ufahamu.

2. Ufupisho (majibu) alama 15)

a)- Adhabu kwa mhalifu.
- Uhalifu na haki. (alama)
(Tathmini majibu ya mwanafunzi)

b) (i) Jela si pahala pa adhabu bali matibabu
(ii) Kifungo kiwe cha kumfunza tabia njema.
(iii) Mhalifu asiadhibiwe kwani jamii imechangia uhalifu wake.
(iv) Muuaji asiuawe,afungwe kifungu cha maisha
(hoja 4x2= alama 8)

c) (i) Muuaji asipouawa hataogopa kuua/ataendelea kuhatarisha maisha ya wanajamii.
(ii) Wanapotukuzwa na magazeti, vitabu na senema wanadumisha uhalifu
(ii)Kutetea "haki" zao kunaongeza uhalifu. (hoja zozote 2x2 (alama 4)

Makosa :

Sarufi – Ondoa makosa 6 yaani alama 3

Tahajia – Ondoa makosa 6 yaani alama 3

M
a-01
b-08
c-04
u+-02
15

3. MATUMIZI YA LUGHA

a) (i) Nomino ya wingi (alama 1)
(ii) Nomino ya kitenzi-jina (alama 1)

b) (i) Ukitia bidii utafaulu (alama 2)
(ii) Mama alisimama babu alipoingia. (alama 2)
Tanbihi.Mwanafunzi akiandika kinyume cha mama na babu apate O


(iii)Hutamuarifu usipomwona. (alama 2)

c.) Mara kwa mara-Kielezi cha idadi cha ujumla
Kijinga - Kielezi cha namna mfanano
Nairobi - Kielezi cha mahali.
Keshokutwa - Kielezi cha wakati
Hobelahobela -Kielezi cha namna kikariri.
Kwa mikono - Kielezi cha namna ala.
Kutaja ½ aina ½ (alama 6)

d) (i) Kiambishi awali cha majina katika kikundi cha KI-VI umoja mf .Kikapu kile cha mama kimepotea
(ii) Nomino katika hali ya udogo mf.kijitabu kimepotea
(iii)kuonyesha masharti mf.ukitaka kufaulu,lazima utie bidii.
(iv) Mianzo ya lugha .mf.Kiswahili kinapendwa sana,Kiluhyia,Kimaasai n.k.
(v)Wakati wa kuendelea.mf.Nilikuwa nikisoma alipofika kwetu
(vi)Kiwakilishi cha majina katika ngeli ya KI-VI. Umoja Kilichonunuliwa kimevunjika.
(vii) Kuonyesha vitendo viwili au zaidi vinafanyika kwa wakati mmoja.
Anakula akilala.

(i) Hutumika kuonyesha vielezi vya namna mfanano
Alitembea kivivu

(e)



½ x 8 = (alama 4)

Yeye ni mchezaji hodari

f) "Msipozinduka na kutetea haki zenu ipasavyo,mtaendelea kudhulumiwa katika nchi yenu . Mwanasiasa mmoja aliwaambia . (⅓ x 9 = alama 3)

g) (i) Mofimu-Kipashio kidogo sana katika lugha chenye maana na ambacho hakiwezi kuvunjwa zaidi. (alama 1)
(ii) Kiambishi-Ni silabi ambayo hufunganishwa na mzizi wa neno ili kulitambulisha neno lenyewe. (alama 1)
(iii) Shadda-Ni mkazo unaowekwa kwenye silabi fulani ya neno ili maana halisi ya neno ijitokeze/Nguvu inayosikika wakati wa kuitamka silabi. (alama 1)

(iv) Kiimbo-Kupanda na kushuka kwa sauti mtu anapoongea. (mawimbi ya sauti)
(alama 1)

h) Ng'ombe ambaye alinunuliwa amekufa
Ng'ombe aliyenunuliwa amekufa.
Ng'ombe mwenye kununuliwa amekufa. (hoja yoyote moja=alama 2)

i)

Kitenzi	Tendewa	Tendesha	Tendeka
Adhibu	Adhibiwa ✗	Adhibisha ✗	Adhibika
Cha	Chiwa ✗	Chisha	Chika ✗

½ x 4 = (alama 2)

j) (i) Kiingizi / kihisishi / kishangao
(ii) Kiunganishi
(iii) kiwakilishi
(iv) Kivumishi.
(v) Kitenzi. (kishirikishi kipungufu)
(vi) Nomino (ya pekee) ½ x 6 = alama 3

k) Watoto- Shamirisho kitondo
Karo - Shamirisho kipozi
Cheki - Shamirisho ala. (hoja 3 x 1 = 3)
(Asiandike kwa cheki kwa kuwa itakuwa kielezi cha namna ala)

l) Maimuna alilionа jinyama lenye majichwa mawili jinyama. (¼ x 4 =alama 1)

ISIMUJAMII (alama 10)

MATATIZO

1. Sera mbovu za lugha katika Wizara ya Elimu na hata shuleni zinazotilia mkazo Kiingereza na kudunisha Kiswahili.
2. Kiingereza kuchukuliwa kuwa chenye hadhi kuliko Kiswahili.
3. Wanaozungumza Kiswahili wanatazamwa kama ni wa tabaka la chini na wenye kisomo duni
4. Matumizi mabaya ya lugha ya Kiswahili katika shughuli mbalimbali na hata vyombo vya habari.
5. Uchache wa magazeti na majarida ya Kiswahili.
6. Kuzuka kwa sheng' miongoni mwa vijana.
7. Athari za lugha ya mama.
8. Uundaji wa istilahi na misamiati ambayo haijasanifishwa.
9. Uhaba wa waalimu wa kufundisha Kiswahili na wataalamu wa kutafiti lugha ya Kiswahili.
10. Uhaba wa vyombo vilivyoundwa na taasisi za kutafiti na kutoa mwongozo kuhusu maendeleo ya Kiswahili
11. Kiswahili kupewa muda mchache katika vyombo vya habari, vipindi vinavyofunzwa shuleni na hata miongoni mwa viongozi hasa bungeni, matumizi hayo ni ya nadra.

12. Uhaba wa vitabu bora vinavyoweza kutumiwa na wanaojifunza kuanzia shule za chekechea hadi vyuo vikuu. Wanafunzi wengi hasa vyuoni na hulazimika kutafsiri vitabu vya Kiingereza.
13. Ushindani mkubwa kutoka kwa lugha nyinginezo kwa mfano Kiingereza, Kifaransa Kijerumani na kadhalika.
14. Kuwepo kwa kasumba ya kikoloni miongoni mwa watu kuihusu lugha ya Kiswahili.

SULUHU

1. Wizara ya Elimu ishughulikie Kiswahili kwa njia sawa na Kiingereza kwa mfano vipindi viongezwe, walimu zaidi waajiriwe, Kiswahili kisifanywe somo la kuchaguliwa na masomo mengine yafunzwe kwa kutumia Kiswahili.
2. Kiswahili kitumike katika nyanja za juu za taifa na shughuli mbalimbali za kitaifa.
3. Raia wahamasishwe na kushawishiwa waionee fahari lugha ya Kiswahili. Wahimizwe kutambua kuwa Kiswahili ni msingi muhimu wa kujitambulisha kama raia wa nchi hii na hata mwenyeji wa Afrika.
4. Shughuli mbalimbali za kiserikali kidini na kisiasa ziendelezwe kwa Kiswahili. Watoao matangazo ya habari wawe waliohitimu vyema katika lugha ya Kiswahili na vipindi vinavyosaidia kukuza Kiswahili vipewe muda zaidi na wakati huo huo vinavyochangia katika matumizi mabaya viondolewe.
5. Serikali ianzishe tuzo za kuwapa waandishi wanaoandika kazi nzuri za Kiswahili.
6. Kuandikwa kwa magazeti na majarida zaidi ya Kiswahili na yauzwe kwa bei ambayo wananchi wanaweza kumudu.
7. Sheng' ipigwe marufuku hasa shuleni na viongozi wawe katika mstari wa mbele katika kuzungumza lugha ya Kiswahili sanifu.
8. Kiswahili kifanywe lugha ya kimsingi katika taasisi za Elimu Kwa mfano, ili ufanye kosi ya uhandisi au udaktari,lazima uwe na umilisi mzuri wa lugha ya Kiswahili. Ili uwe kiongozi hata wa kisiasa lazima uelewe Kiswahili.
9. Serikali itenge kiasi fulani cha fedha ili kuendeleza Kiswahili katika taasisi za elimu. Walimu wa Kiswahili wapewe/waongezewe marupurupu maalum ili kuwahimiza wengi wasomee lugha hii.
10. Serikali izuke na vivutio vya kuwapa wachapishaji wa makala mbalimbali ya Kiswahili. Hazina maalum ya fedha itengwe kuwasaidia waandishi wanaofanya utafiti na kuandika lugha ya Kiswahili. Wataalamu wa lugha na wale wenye ujuzi wa kina wa lugha washirikishwe katika tafiti muhimu za lugha.
11. Vipindi vya redio na runinga ambavyo vinahimiza matumizi fasaha ya Kiswahili shuleni viongezwe,vipindi vya Kiswahili viongezwe na hata serikali iwaajiri walimu zaidi wa Kiswahili.
12. Wachapishaji na waandishi wahimizwe kutoa machapisho ya lugha ya Kiswahili ili vitabu zaidi viandikwe kuwasaidia wanaojifunza.

Makosa :

Sarufi – usiondoe makosa zaidi ya nusu ya alama alizopata katika sehemu nzima. (Mfano, akipata alama 6 jumla utatoa makosa 6 yaani alama ½ x 6 = 3 ya sarufi.

Tahajia – ondoa makosa 6 yaani alama 3

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2

LUGHA

JULi-2010

MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA MKOA WILAYANI THIKA

MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA

MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA

UFAHAMU.

A. Silaha ya uhalifu (alama 1)

B. Unaweka wazi namna ambavyo yowe linaweza kuwa silaha ya kumaliza uovu katika jamii. (alama 2)

C. Utaifa/umoja katika nchi- Watu kujumuika pamoja.
Uchumi-malipo ya wachezaji na washiriki wengine
Starehe/burudani – mashabiki.
Amani/Usalama-vijana wanakuwa na linalowashughulisha. (alama 4)
Zozote 4 x 1

D.i Dhuluma dhidi ya haki za watu
ii. ubakaji
iii. Dhuluma iletwayo na tamaduni mbovu.
iv. Biashara mbovu ya kichawi na haramu.
v. Njia mbovu ya vikosi vya usalama kupokea habari.
4 x ½

Zozote nne x ½

E.i. Si hoja waonekanavyo nje: wabaya au wazuri.
ii. Sharti ukweli usemwe ili pasiwepo hali ya sintofahamu. (alama 2)

Fi Kuwadanganya/kuwalaghai/kuwahadaa.
ii. alipomshuku/ (alama 2)

G.i. Balagha mfano Aya 2 na 3
ii. Uhuisho/ Tashhisi- mf mchezo wa kandanda umenifunza jambo.
iii. Ishara-yowe ishara ya kutiridhika/kuridhika.
(alama 2)
Zozote 2 x 1

UFUPISHO.

(a)i. Hufungua vitundu vya ngozi
ii. Husaidia kuondoa sumu mwilini kupitia kwa utokaji jasho
iii. Kupunguza mikazo ya misuli. Mikazo ya misuli mwilini kwa muda mrefu huleta ulundikaji wa asidi mwilini jambo ambalo ni hatari.
iv. Huondoa uchovu na kuleta uchangamfu mwilini.
v. Huimarisha mzunguko wa damu mwilini kwa wepesi.
vi. Hurahisisha virutubishi vya mwili kufikia sehemu zote mwilini.
vii. Ukandaji huchangamsha neva na kuimarisha utendaji kazi wa neva hizo.
7 x 1. 7 2 mtiririko.

(b)i Viganja vya mikono hutumika katika ukandaji na vinapaswa kuwa na wororo kutokana na matumizi ya mafuta.
ii. mafuta hutumika katika ukandaji hasa ya ufuta au simsim.
iii. Mtu aanzie mikononi na miguuni, aingie kifuani, tumboni, mgongoni na makalioni.
iv. Aingie usoni na kumalizia kichwani, iwapo anayehusika hana tatizo la afya.
v. lkiwa anayehusika ana tatizo la shirikizo la damu, utaratibu uanzie kichwani kisha aelekee usoni, kifuani, tumboni na kumalizia mgongoni.
5 x 1 5, 1 mtiririko

MATUMIZI YA LUGHA

A. nuia, zuia, maua n.k (alama 1)
Bi. Kutanguliza maelezo/usemi. Mfano :
Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa__ aliyefika hapa nchini leo asubuhi__atafanya mashauri.
ii. Kutoa maelezo zaidi kuhusu kinachotajwa, mfano Tunahitaji pembejeo za kilimo – jembe la kukokotea, tingatinga na vinyunyizaji maji.
iii. Kuonyesha ni nani aliyesema maneno fulani.
Mfano: Majambazi wote wasakwe – Rais
(zozote mbili za mwanzo)
(alama 2)
C. ghafilika (sahau) ghafilikika. (alama 2)

D. <u>Mtue</u> Bi. Kizee mtungi huu wa maji. (alama 1)

E.

	S		
KN ½		KT ½	
N ½	T ½	KN ½	
		N ½	S ½
Polisi	wamekamata	jambazi	aliyesumbua watu ½

(alama 4)

Au

S				
KN ½	KT ½			
N ½	T ½	N ½	T ½	N ½
Polisi	wamekamata	jambazi	aliyesumbua	watu ½

(alama 4)

F. Wanafunzi wengi- Kirai nomino
Katika michezo – Kirai kihusishi. (alama 2)

G. Kinyama/kijinyama kilicho katika kigome/kijigome kile hakina kikia/kijikia. (alama 2)

H. Kameme alishangaa kuwahusu wanawe na kuwauliza kulikuwa na nini walielekea kutoelewa jambo rahisi kama hilo. (alama 2)

I. A.- Kiambishi cha nafsi/Ngeli
li -Kiambishi cha wakati uliopita
ji kirejeshi
nyw- mzizi
i - Kauli ya kutendea
a- kiishio
(alama 3)

J. Akomeleapo/Anapokomelea mwenyeji na mgeni koma papo. (alama 2)

K(.i) Amefanya kazi hiyo barabara. E
(ii) Barabara! Mambo yamekwenda kama tulivyotarajia. (alama 2)
I

L. Nenepesha (alama 1)
Taifisha (alama 1)

M. Mayai - Kipozi
Mkata- Kitondo (alama 2)

N(i). Kaka wa mama

ii). Mtu wa pwani kama aitwavyo na watu wa bara: Mswahili.
bara: Mswahili.

iii). Aina ya samaki

(alama 3)

O. kilicho- kishirikishi kipungufu.
si – kishirikishi kipungufu

(alama 2)

P. Ambatano ni sentensi mbili sahihi zilizowekwa pamoja kwa kutumia kiunganishi.
Mf.: Baba analima na mama anapika.
Changamano hutumia kishazi huru na kishazi tegemezi
Mf: <u>Mwanafunzi</u> aliyesoma <u>amefaulu.</u>
Mwanafunzi amefaulu- Kishazi huru.
Amefaulu – Kishazi tegemezi. (alama 4)

Q. U- hutoweka katika wingi mf uteo-teo
U- NY – ua – nyua
U-ND – ulimi – ndimi
W-NY- Wimbo – nyimbo
U – MB – ubao – mbao (alama 2)

R. <u>Iyo hiyo</u> ilipandwa jana. (alama 2)

ISIMU JAMII

A. <u>Njia za kueneza</u>

i. Misafara ya watu waliokuwa wakishiriki katika biashara baina ya pwani na sehemu za ndani. (bara)
ii. Maingiliano ya watu waliokuwa na haja ya kuwasiliana katika biashara ya watumwa, pembe za ndovu n.k
iii Sababu za kisiasa baadaye hasa Kenya ilipokuwa ikitawaliwa na wakoloni.
iv. Juhudi za usambazaji wa dini ya Kiislamu na pia dini ya Kikristo miongoni mwa wenyeji.
v. Baadaye matumizi ya vyombo mbalimbali vya habari.

5 x 1

B

